

HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA



TANGAZO LA ZABUNI

ZABUNI Na. LGA/128/2018-2019/HQ/NC/10

ZABUNI YA UWAKALA WA KUTOA HUDUMA YA USAFI WA KUZOA TAKA KUTOKA KATIKA KATA 16 ZA KATIKATI YA JIJI NA KUKUSANYA ADA YA TAKA NGUMU KUTOKA KWENYE KAYA, TAASISI NA MAJENGO YA BIASHARA KATIKA JIJI LA TANGA.

1. UTANGULIZI

Halmashauri ya Jiji la Tanga inawatangazia zabuni za kutoa huduma ya **kukusanya taka na kuzisafirisha hadi katika dampo rasmi na kukusanya ada ya taka** katika Kaya, Taasisi na majengo ya biashara kwa mujibu wa sheria ndogo za udhibiti mazingira za Halmashauri ya Jiji la Tanga za mwaka 2014 na marekebisho yake. Kupitia Zabuni hii Halmashauri inakusudia kupata mzabuni/Wazabuni (Kampuni) mwenye/wenye sifa na uwezo wa kutoa huduma hii.

2. KAZI ZITAKAZOFANYIKA

Mshindi wa Zabuni hii atapatiwa Mkataba wa **kukusanya taka na kuzisafirisha hadi katika dampo rasmi na kukusanya ada ya taka ngumu** katika Kaya, taasisi na majengo ya biashara ndani ya Kata husika kwa mujibu wa sheria ndogo za halmashauri za udhibiti uchafuzi mazingira za mwaka 2014 na marekebisho yake.

Pamoja na kazi hizi, Wakala atatakiwa kutekeleza majukumu mengine ikiwa ni pamoja na kuwasilisha taarifa za utekelezaji na vielelezo vingine kwa mujibu wa taratibu za halmashauri ya Jiji la Tanga na pia kwa mujibu wa mkataba atakaokuwa amekubaliana na Halmashauri ya Jiji la Tanga.

3. MAENEO YA ZABUNI (KATA)

Maeneo yaliyopangwa kwaajili ya kupatiwa huduma hii ni:

Na.	Jina la Kata	Idadi ya Kaya	Idadi ya majengo ya biashara
ZABUNI NA. LGA/128/2018-2019/HQ/NC/10 – LOT 03			
1.	Central	432	333
2.	Ngamiani Kaskazini	433	339
3.	Ngamiani Kati	393	522
4.	Ngamiani Kusini	1542	27
5.	Majengo	543	192
6.	Chumbageni	944	631
7.	Nguvumali	2296	288
8.	Msambweni	694	67

Na.	Jina la Kata	Idadi ya Kaya	Idadi ya majengo ya biashara
ZABUNI NA. LGA/128/2018-2019/HQ/NC/10 – LOT 04			
9.	Mwanzange	802	165
10.	Makorora	320	128
11.	Usagara	1920	115
12.	Mzingani	1306	202
13.	Duga	550	27
14.	Mabawa	1390	91
15.	Mnyanjani	998	254
16.	Magaoni	264	68

4. MAKABRASHA YA ZABUNI

Makabrasha ya Zabuni ikiwa ni pamoja na Hadidu za rejea na vielelezo vingine muhimu vinapatikana katika Ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni ya Halmashauri ya Jiji iliyopo katika jengo la Makao makuu ya Halmashauri ya Jiji la Tanga (Twiga), chumba namba 06. Aidha, kila mwombaji atapaswa kulipa kiasi cha shilingi **100,000/=** Ili kuweza kupata Kabrasha la Zabuni hii.

Pamoja na ilivyoelekezwa kwenye Maelezo ya Mahitaji katika ukurasa wa pili wa kabrasha la zabuni hii, maombi yatakwawasilishwa yawe pia na taarifa muhimu za mwombaji zifuatazo:

- Anuani, mahali Ofisi ilipo, namba ya simu na e-mail,
- Vifaa vya usafi alivyo navyo kwa kazi aliyoomba,
- Wataalamu alionao (elimu na ujuzi wao),
- Uwezo wa kifedha utakaothibitishwa na benki
- Uzoefu alionao katika utoaji wa huduma za usafishaji

5. UWASILISHAJI WA ZABUNI

Zabuni zote ziwe na nakala halisi (original) 1 na (copy) 2 zinazofanana, ziwekwe kwenye bahasha iliyofungwa vizuri na kuandikwa kwa usahihi “**Zabuni Na. LGA/128/2018 – 2019/HQ/NC/10 KUTOA HUDUMA YA UDHIBITI TAKA NA USAFI KATIKATI YA JIJI LA TANGA**” na yatumbukizwe kwenye sanduku la zabuni lililopo **OFISINI KWA KATIBU WA BODI YA ZABUNI** wa Halmashauri ya Jiji la Tanga S.L.P 178, Tanga, Chumba Na. **06**.

6. UFUNGUZI WA ZABUNI

Mwisho wa kupokea zabuni ni tarehe 17/1/2019 saa 10:00 asubuhi, na zabuni zitafunguliwa tarehe 17/1/2019 muda mfupi baadae kwenye Ukumbi wa jengo la makao makuu ya Halmashauri ya Jiji la Tanga. Wazabuni watakaopendelea kushuhudia ufunguzi wa zabuni hizo wanakaribishwa kuwepo muda huo.

Imetolewa na:

**MKURUGENZI
HALMASHAURI YA JIJI
TANGA**